**JIMBO KATOLIKI LA MOROGORO**

**SHULE YA SEKONDARI ALFAGEMS**

**S.L.P 6083 MOROGORO**

## UTUSAIDIE KUOKOA ALFAGEMS

Ndugu,

shule yetu pendwa inakabiliwa na tishio la kupigwa mnada kwa sababu imechelewa kurejesha pesa iliyokopa benki kutokana na matatizo mbalimbali pamoja na kuanza ununuzi wa shule ya sekondari Denis.

Tunachohitaji haraka sana ni kutoka katika uchefuchefu wa kibenki kwa kurejesha sehemu kubwa ya pesa zilizotakiwa mnamo 10 Oktoba 2024, milioni 130 hivi. Baada ya hapo tutaweza tukakubaliwa taratibu mpya na nafuu za kurejesha mkopo.

Kwa ajili hiyo tunaomba wafanyakazi wa Alfagems, wazazi, wanafunzi wa zamani na wengineo waingize kiasi chochote wanachoweza katika akaunti ya Benki ya Mkombozi yenye jina la shule na namba 00120603517801 halafu kututumia picha ya malipo kwa njia ya Whatsapp katika simu ya uhasibu wa shule namba 0685-701614.

Kutokana na malipo haya utachagua mwenyewe kati ya hayo matatu:

1. Kuhesabiwa hizo pesa kama ada ya mwanafunzi fulani kwa ajili ya siku zijazo.
2. Kurudishiwa hizo pesa mwaka ujao ukiongezewa 10% kama shukrani.
3. Kuandikishwa kama mwanahisa wa kampuni itakayoanzishwa ili kumiliki na kuendesha shule ya Denis ambayo thamani yake ya sasa ni kama bilioni 1.2 lakini kwa kila milioni utakayochangia utakuwa mmiliki wa asilimia 0.1%.

Tunaomba ufikishe mapema ujumbe huu kwa wengine watakaoweza kutusaidia kuokoa shule hii isiuzwe.

Kwa taarifa zaidi, wasiliana nasi kupitia simu namba 0685-701614.

Mungu akubariki na kukujalia amani!

Nd. Rikardo Maria, UNWA, meneja